# Hadithi 9

# KUMPWEKESHA ALLAH KATIKA MATENDO YAKE

Kutoka kwa Imran bin Huswein, Mwenyezi Mungu awe radhi nao, amesema:

1 Niliingia kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) nikamuacha ngamia wangu mlangoni.

2 Wakamjia Mtume baadhi ya watu katika familia ya Tamim, akawaambia: “pokeeni bishara enyi familia ya Tamim.”

3 Wakasema familia ya Tamim: Umetubashiria, basi tupe mara mbili.

4 Kisha wakaingia baadhi ya watu wa Yemen, Mtume akasema: pokeeni Bishara enyi watu wa Yemen, kwani familia ya Tamim hawakuikubali”.

5 Wakasema watu wa Yemen: Tumeikubali, ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu.

6 Wakasema watu wa Yemen: Tumekuja kukuuliza kuhusu hili jambo (la Uislamu).

7 Akasema Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake): “Mwenyezi Mungu alikuwepo, wakati hakuna chochote kilicho kuwepo ispokuwa yeye.

8 Na Kiti chake cha enzi kilikuwa juu ya maji.

9 Na akaandika katika kitabu kila kitu.

10 Na akaumba mbingu na ardhi”.

11 Akaita Muitaji akasema: Ngamia wako ametoweka, ewe Ibn al-Huswein, basi nikaondoka mbio nikimtafuta, Ghafla nikamuona akitokomea kwa umbali.

12 Wallahi, nikatamani laiti ningemuacha”[1].

1 Al-Bukhari (3191).

## Ayah

Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

- *﴿Ni Yeye ndiye aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Na Kiti chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji﴾ [Hud: 7].*
- *﴿Hakika Sisi tunawafufua wafu, na tunayaandika wanayo yatanguliza, na wanayo yaacha nyuma. Na kila kitu tumekihifadhi katika Kitabu chenye kubainisha﴾ [Yasin: 12].*
- *﴿Sema: Hivyo nyinyi mnamkataa aliye umba ardhi katika siku mbili, na mnamfanyia washirika? Huyu ndiye Mola Mlezi wa walimwengu wote (9) Na akaweka humo milima juu yake, na akabarikia humo na akakadiria humo chakula chake katika siku nne. Haya ni sawa kabisa kwa wanao uliza (10) Kisha akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi, akaziambia hizo na ardhi: Njooni, kwa khiari au kwa nguvu! Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni wat'iifu (11) Basi akazifanya mbingu saba kwa siku mbili, na akazipangia kila mbingu mambo yake. Na tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua﴾ [Fussilat: 9-12].*
- *﴿Kwa hakika Sisi tumekiumba kila kitu kwa kipimo﴾ [Al Qamar: 49].*

## Msimulizi

Yeye ni: Imran bin Husayn bin Obaid Al-Khuza'i, Abu Nujaid, alisilimu mwaka wa 7 Hijiriya, na alikuwa kiongozi alieshikilia bendera ya ukoo wa Khuza'ah siku ya ufunguzi wa makkah. Umar ibn al-Khattab Mwenyezi Mungu awe radhi naye alimtuma Basra huko Iraq, ili kuwafundisha watu dini yao, naye alikubali agizo hilo, na hakushuhudia fitna, alifariki mwaka wa 53 Hijiria[1].

## Muhtasari

Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) anaeleza kuhusu baadhi ya mambo ya siri yanayobainisha sifa na matendo ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, na ameeleza kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa wa milele kabla ya kila kitu, na arshi yake ilikuwa juu ya maji kabla ya kuumba mbingu na ardhi. Kisha akasema kuwa Mwenyezi Mungu aliandika katika Kitabu kilichohifadhiwa, makadirio ya waja na matukio yote, baada ya hapo akaumba Mbingu na Ardhi.

1 Rejea tafsiri yake katika: “Maarifaat al-Sahaba cha Abu Naim” (1/38), “Asad al Ghaba cha Ibn al-Atheer” (4/137), “Al-Isbah cha Ibn Hajar” (4/484).)

# Ufahamu

1. Imran bin Al-Husein Mwenyezi Mungu amuwie radhi aliingia kwa Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) na akafunga ngamia wake ili asitoroke wala kukimbia.

2. Alipokuwa amekaa na Mtume likaingia kundi la kabila la Tamim, akasema Mtume kuwaambia: “pokeeni bishara” na ilikuwa jambo zuri kwao ni kupokea bishara hiyo kwa kuwa inatoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) hata kama itakuwa kiasi kidogo namna gani, hususani kuwabashiria kuwa atakayesilimu hatabaki motoni milele...[1].

3. Familia ya Tamim waliposikia bishara hiyo walidhani ni katika mambo ya kidunia nyoyo zao zikaelekea huko, wakasema: “Umetubashiria, basi sasa tupe, wakasema mara mbili. Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) aliwakasirikia kwa kusema hivyo, na kutokujali bishara hiyo, na wakawa na matamanio ya Dunia yenye kuondoka, na walijua bishara njema ni utoaji wa mali tu.

4. Baada ya hayo wakaingia kwake watu wa Yemeni, ni maash’ariy Watu wa Abu Musa Al-Ash’ari, akawaambia Mtume: “Pokeeni bishara, kwani familia ya Tamim hawakukubali. Japo kuwa familia ya Tamim walisilimu, lakini kwa sababu ya ugeni katika Uislamu wakati huo, habari njema hawakuikubali kama inavyo takikana, kwa kuwa waliweka sharti la kuikubali bishara hiyo wapewe mali[2].

5. Watu wa Yemen walikuwa wajuzi zaidi kuliko familia ya Tamim, kwa hivyo walizikubali bishara hizo bila vikwazo wala matakwa, na ndio maana Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) alisema: “Imani iko Yemen, na busara inapatikana ndani Yemen”[3].

6. Kisha baada ya kukubali bishara, walimuuliza Mtume wa Mwenyezi Mungu (Rehma na Amani ziwe juu yake) kuhusu ulimwengu huu au viumbe wanavyoviona. Haikuonekana katika swali kile walichouliza, lakini ilijulikana kupitia jibu Lake Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake).

7. Mtume Rehema na Amani zimshukie alijibu swali lao kuwa Mola Mtukufu ni wa tangu enzi na enzi na hakuna chochote kilichokuwepo pamoja naye katika dunia hii, si mbingu wala ardhi, na hii haimaanishi kutokuumbwa vitu kabla ya mbingu na ardhi. Kwani Arshi iliumbwa kabla ya hapo na ipo. kama hadithi inavyoonyesha, na Mwenyezi Mungu huumba apendavyo[4].

---

1 Tazama: Fath al-Bari cha Ibn Hajar (13/409).

2 Tazama: Fath al-Bari cha Ibn Hajar (13/409).

3 Al-Bukhari (3499) na Muslim (52).

4 Majmuu’ al-Fatawa cha Ibn Taymiyyah na linganisha: Fath al-Bari cha Ibn Hajar (6/289).

8 Kisha akawaambia kwamba Arshi ya Mwenyezi Mungu Mtukufu ilikuwa juu ya maji kabla ya kuumba mbingu na ardhi, kama Mwenyezi Mungu Mtukufu alivyosema katika qur`an: “Ni Yeye ndiye aliyeumba mbingu na ardhi katika siku sita. Na Kiti chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji” [Hud: 7]. Na alipomaliza kuumba mbingu na ardhi akatulizana katika Arshi juu ya mbingu. Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema: “Mola wenu Mlezi ndiye aliye umba mbingu na ardhi katika siku sita, kisha akatawala juu ya arshi” [Al-Aaraf: 54].

Kiti cha Enzi cha Mwingi wa Rehema ni cha juu zaidi, na ni kikubwa na kitukufu kuliko viumbe vyote, na Arshi makusudio yake ni kiti cha ufalme.

9 Kisha Mtume (Rehma na Amani ziwe juu yake) akabainisha kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu aliandika hukumu za waja na yanayotokea ulimwengu mzima katika kitabu – Ubao- kilicho hifadhiwa, imepokelewa kutoka kwa Abdullah bin Amr bin Al-Aas. Amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu Amani Iwe juu yake akisema: “Mwenyezi Mungu aliandika hukumu za viumbe kabla hajaumba mbingu na ardhi. Kwa Miaka hamsini elfu, alisema: Kiti chake cha enzi kiko juu ya maji[1].

10 Kisha akamwambia Mtume Rehema na Amani zimshukie kuwa Mwenyezi Mungu ameziumba mbingu na ardhi baada ya kuumba maji na arshi na kuandika hukumu za viumbe katika Ubao Uliohifadhiwa. Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amelieleza jambo hilo akisema: “Sema: hivi nyinyi mnamkataa aliye umba ardhi katika siku mbili, na mnamfanyia washirika? Huyu ndiye Mola Mlezi wa walimwengu wote (9) Na akaweka humo milima juu yake, na akabarikia humo na akakadiria humo chakula chake katika siku nne. Haya ni sawa kabisa kwa wanao uliza (10) Kisha akazielekea mbingu, na zilikuwa moshi, akaziambia hizo na ardhi: Njooni, kwa khiari au kwa nguvu! Vyote viwili vikasema: Tumekuja nasi ni wat’iifu (11) Basi akazifanya mbingu saba kwa siku mbili, na akazipangia kila mbingu mambo yake. Na tukaipamba mbingu ya chini kwa mataa na kwa ulinzi. Hichi ndicho kipimo cha Mwenyezi Mungu Mwenye Kujua” [Fussilat: 9-12].

11 Kisha mtu akamwambia Imran kuwa ngamia wake ametoroka kutoka kwenye kamba na kukimbia, basi Imran akatoka kwenda kumuona, na kukuta kishatoweka machoni mwake, na kukawepo uzio baina yake na Ngamia. Ni uzio ambao huonekana jangwani kwenye joto kali kana kwamba ni maji.

12 Imran alisikitika kuondoka kwake kutoka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, amani iwe juu yake; Ambapo aliinuka na hakusikia Hadithi iliyobaki kutoka kwa Mtume Amani iwe juu yake.

1 Muslim (2653).

# Mafunzo

1. Imran bin Husein alimfunga ngamia wake kwenye mlango wa Msikiti wa Mtume Amani iwe juu yake, na hii inaonyesha namna ya kumtegemea Mwenyezi Mungu, katika suala la kuchukua sababu na kumtegemea Mwenyezi Mungu. Hakusema: Nimwache Ngamia bila kumfunga na nimtegemee Mwenyezi Mungu.

2. Mtume Rehema na Amani zimshukie, alipenda kuwabashiria maswahaba zake, basi pambeni mazungumzo yenu mnapozungumza na watu kwa kila aina ya bishara, kama vile bishara ya yale aliyowaandalia Mwenyezi Mungu kwa watu wa imani. na subira kutokana na Pepo iliyo karibu na ijayo, Na katika bishara njema ni kuwaondoshea watu majonzi na khofu, na ni juu ya Waalimu wasiishie kueleza hukumu za fiqhi, mafundisho na nyenginezo bila ya kuzungumza na Nafsi.

3. Ushindi wa Akhera ni wakipekee, na ndio maana Mtume Rehema na Amani zimshukie, akawakasirikia Banu Tamim kwa kuwa hawakutosheka na bishara hiyo na wakaomba Mali ambayo inakomea duniani tu. Je, tunapoteza kiasi gani pale ambapo tunatanguliza malipo ya Dunia na kuisahau Akhera.

4. Usione haya kuuliza katika mambo ya Dini, sawasawa kuuliza juu ya hukumu za Sharia na yaliyo halali na haramu, au kuhusu hali halisi ya Kiyama na khabari za mataifa yaliyotangulia.



5 Mfikirie kwa uzuri Mola wako Mlezi; Ana uwezo wa kukupatia kile unachotamani; Je, hivi aliyeumba ulimwengu mkubwa namna hii na kuushika mkononi mwake, hana uwezo wa kuitikia wito wako?!

6 Iwapo Mwenyezi Mungu Mtukufu alikwisha andika hukumu za uumbaji kabla ya kuumbwa mbingu na ardhi, basi haifai kwa mja kuomboleza kwa yale aliyoyakosa kwa yale aliyokuwa akiyatarajia katika kheri, na wala asiwe na wasiwasi juu yake. nini kilimtokea kwa yale aliyokuwa anaonya juu ya uovu, kwa sababu kama mtumishi alifanya hivyo, alikuwa amechukizwa kulingana na amri ya Mungu.

7 Imran bin Huswein radhi za Mwenyezi Mungu zimshukie alijuta alipotoka nje akimwangalia ngamia wake na kuacha Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu Amani iwe juu yake, Majuto Hayo yanaashiria ubora wa elimu ya Kiislamu, na kwamba kuipata na kifahamu kwake ni bora kuliko kujishughilisha na Dunia na vilivyomo. Haifai kwa mwenye akili timamu kupuuza Ubora huo.



